



# KANUNI ZA KIJAMII: RASILIMALI KWA UTUME NA HUDUMU



## JUMUIYA YA KIUCHUMI

Sehemu ya Jumuiya ya Kiuchumi imegawanywa katika sehemu tatu: dibaji, ambayo inaunganisha somo na historia ya Wesley, maandiko, na teolojia; Changamoto za Kiuchumi, ambazo zinaelezea matatizo ya kiuchumi ya kimataifa tunayokabiliana nayo leo; na Haki ya Kiuchumi, ambayo inafafanua ahadi yetu ya kuunda uchumi wa haki na endelevu.

Masuala yailiojumuishwa katika Jumuiya ya Kiuchumi:

- Utandawazi
- Umaskinina Mapato Yasio Sawa
- Biashara Haramu ya Binadamu na Utumwa
- Hongo na Ufisadi
- Sabato na Wakati wa Upya
- Utumiaji wa Kuwajibika
- Kilimo na Uzalishaji wa Kilimo
- Heshima ya Kazi
- Majukumu ya Kampuni

## Soma na uzungumze Jumuiya ya Kiuchumi

*Tumia maswali yafuatayo kuongoza mafunzo yako ya kibinafsi au kuongoza vikao vya vikundi vidogo ndani ya kanisa lako. Sisitiza jinsi masuala yanahusiana na kanisa lako na eneo lako, ukizingatia picha kubwa ya kimataifa.*

### Tafuta Njia za Kuondoka Kutoka Maneno hadi Utezezi Kutafsiri Imani Kuwa Vitendo

- Ni ukosefu gani wa haki wa kiuchumi unaotawala mahali unapoishi?
- Ni baadhi ya njia zipi ambazo Kanisa linaweza kushughulikia masuala haya kupitia mipango ya msingi, kupanua huduma za sasa, kujihusisha na mashirika ya kijamii, na kutetea mabadiliko ya sera?
- Soma Amosi 5:7-13, Mathayo 25:3-46, na Yakobo 2:15-16. Ni kwa jinsi gani kanisa linaweza kuongeza mwitikio wake kwa tatizo la ukosefu wa haki wa kiuchumi kwa kujihusisha na kuunga mkono "wale walioonekana kuwa si watu wa thamani" katika jumuiya yetu, na ni hatua gani za kivitendo tunaweza kuchukua ili kuhakikisha kwamba juhudi zetu zinakuza mabadiliko ya kudumu na ya usawa kwa wale wanaohitaji zaidi?
- Angalia kukosekana kwa usawa wa kiuchumi duniani na athari zake kwa jamii. Matendo ya jumuiya yako yanawezaje kuathiri jumuiya zaidi ya mazingira yako ya karibu?

### Rasilimali nyingine:

John Wesley, "Matumizi ya Pesa"

Kadi za Imani na Ukweli (zilisasishwa na kutolewa mwaka wa 2025)

Mpango wa Vijana wa Imani na Haki (zilisasishwa na kutolewa mwaka wa 2025)

Ukurasa wa Haki ya Kiuchumi wa GBCS:

<https://www.umcjustice.org/what-we-care-about/economic-justice>

